**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**6 Novemba 2024**

# TAARIFA KWA UMMA

Taarifa inatolewa kwa umma kuwa kufuatia uamuzi wa Access Bank (Nigeria) Plc kununua asilimia tisini na sita ya hisa za African Banking Corporation Tanzania Limited, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa idhini kwa African Banking Corporation Tanzania Limited kubadilisha jina lake na kuitwa Access Bank Tanzania Limited. Hivyo basi, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni ya benki kwa ***Access Bank Tanzania Limited*** kuanzia tarehe 19 Septemba 2024.

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**